**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**Simu Nam. + 255 24 2230602/1**
**Fax Nam. + 255 24 2230215**
**Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz**

**SANDUKU LA BARUA 902,**
**ZANZIBAR**
**Barua Pepe: zahore@zanlink.com**

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu (S.A.W), Mwingi wa Rehma, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo, kwa kutujaalia kukutana kwa mara nyengine tena katika Baraza la Kumi kwa dhamira ya kujadili Bajeti kuu ya Serikali na taasisi zake katika Baraza lako Tukufu. Kwani hii ni rehma yake Muumba kwa kutupa pumzi na afya njema ambayo wenzetu wengine amewanyima fursa hii.

**Mheshimiwa Spika,** pia, napenda kutumia fursa hii adhimu kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu, kwa lengo la kuwasilisha maoni ya *Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa* kuhusiana na *Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ* kwa mwaka wa fedha *2021/2022* kama Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020 zinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, nawapongeza na kuwashukuru kwa dhati viongozi wa Wizara hii wakiongozwa na Waziri wao Mheshimiwa Masoud Ali Mohammed, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Mikoa pamoja Afisa Mdhamini Pemba na watendaji wote kwa mashirikiano yao makubwa waliyotuonesha katika Kamati yetu na kupelekea kutekeleza majukumu yetu ipasavyo. Vile vile, shukurani za pekee ziende kwa Wakuu, Maafisa na Wapiganaji wote wa Vikosi vya Idara Maalum za SMZ kwa mashirikiano yao waliyotupatia kwa kipindi chote cha utekelezaji wa shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hayo, natumia nafasi hii kuishukuru Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kutumia na kutekeleza vyema ushauri na maagizo ya Kamati pamoja na kusimamia kwa ukamilifu na ufanisi utekelezaji wa Bajeti yao ya mwaka *2020/2021*, jambo hili limewawezesha kujenga ari ya kuwasilisha mbele ya Kamati yetu, pamoja na Baraza lako Tukufu Makadirio mapya ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa fedha *2021/2022* ili yapate baraka za Wajumbe wako na kwa madhumuni hayo, tunaliomba Baraza lako liridhie na liipitishe Bajeti hii kwa maslahi ya wananchi na Serikali kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, naomba kutoa shukrani na pongezi za pekee kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi imara wa Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika uongozi wake na kuhakikisha maendeleo ya watu na ustawi wa jamii nchini umeimarika pamoja na kusimamia maendeleo ya kiuchumi kufuatana na misingi na madhumuni yaliyowekwa katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka *1984*, kwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora unafanikiwa kwa wananchi wote wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** ni matumaini ya Kamati yangu kuwa, mafanikio yanayopatikana katika uimarikaji wa uchumi wetu na huduma za kijamii yanatokana na utekelezaji mzuri wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka *2020/2025.*

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti hii imekadiriwa kufanya kazi kwa kuzingatia malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na inaakisi hali halisi ya uchumi wetu na harakati za kupunguza umasikini lakini pia kwa kuzingatia malengo ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** pia, nachukua nafasi hii kuwashukuru kwa kazi kubwa waliyoifanya Wajumbe wa Kamati yangu wakati tulipoipitia bajeti hii, kwa kuonesha umahiri na mashirikiano yao makubwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati hii.

Hivyo, kwa ridhaa yako naomba sasa uwatambue Wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Hassan Khamis Hafidh | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Machano Othman Said | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *7.* | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| *8.* | Ndg. Haji Jecha Salum | Katibu |
| *9.* | Ndg. Salma Muhsin Haji | Katibu |
| *10.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imetumia uweledi wake wa hali ya juu katika kupitia, kuchambua na kujiridhisha vyema na programu zote zilizokusudiwa kufanyiwa kazi kupitia Mafungu ya Bajeti ya Wizara hii kama ilivyoelezwa katika Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka *2020*.

**Mheshimiwa Spika,** ni imani ya Kamati hii kwamba kupatikana kwa fedha zilizopangwa katika Wizara hii kutasaidia kwa kiasi kikubwa utekelezaji na ukamilishaji wa malengo yaliyokusudiwa kutekelezwa ikiwa ni pamoja na kukamilisha miradi iliyotengwa katika bajeti hii ya mwaka wa fedha *2021/2022* na vile vile kumalizia mradi mkubwa wa ujenzi wa mahanga na nyumba za askari wa Idara Maalum Unguja na Pemba.

## PROGRAMU ZA MAKAO MAKUU (FUNGU D 01)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa kuna tatizo katika Sheria ya Jumuiya zisizo za Kiserikali, nambari 6 ya mwaka 1995 kuwa imepitwa na wakati na kupelekea kupunguza ufanisi wa utendaji wa kazi zetu za kila siku.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuharakisha na kukamilisha mapitio ya Sheria ya Jumuiya Zisizo za Kiserikali, nambari 6 ya mwaka 1995 ambayo inaonekana kupitwa na wakati na kupelekea baadhi ya watu kuunda na kuendesha Jumuiya kinyume na taratibu za nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto za wafanyakazi, stahiki zao pamoja na wataalamu wa uendeshaji wa mashine katika Viwanda vya Nguo na Viatu vya Idara Maalum za SMZ.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Wizara izidi kuchukua juhudi za kuhakikisha kuwa Viwanda vya Nguo na Viatu vilivyo chini ya Vikosi vinafanya kazi ipasavyo na vinaleja tija. Aidha, Kamati inaiomba Wizara kuendelea kuwajengea uwezo wa kitaalamu na kifedha wasimamizi na watendaji wa Viwanda hivyo ili lengo la Serikali la kuanzisha Viwanda vya Idara maalum liweze kutimia. Pia, juhudi za kuvitangaza Viwanda hivyo zinahitajika ili viweze kujiendesha vyenyewe hapo baadae.

## PROGRAMU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ (FUNGU D 02 – D 06)

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inawapongeza Wakuu wote wa Vikosi walioteuliwa hivi karibuni na kuwataka wafanye kazi kwa uadilifu ili kuvifanya Vikosi hivyo kuwa na nidhamu katika utekelezaji wa majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhishwa na juhudi zinazofanywa na wapiganaji wetu wa vikosi kwa kazi nzito wanazozifanya za kulinda, kusimamia na kudumisha usalama wa raia na mali zao pamoja na kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto za kiutawala na uwajibikaji katika baadhi ya vikosi vya SMZ pamoja na matumizi yasiyoridhisha katika utekelezaji wa miradi mbali mbali katika Vikosi vyetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini hakuna vitendea kazi bora na vinavyokwendana na wakati kwenye vikosi vyetu jambo ambalo linapelekea kushindwa kufanyakazi zao kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kulitafutia ufumbuzi suala la uhaba wa vitendea kazi kama vile rada katika kambi ya KMKM Masingini, Unguja na Sengenya, Pemba pamoja na vitendea kazi vyengine kama vile vyombo vya usafiri na mafuta ya kutosha kwa ajili ya vyombo hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini maslahi wa wapiganaji wetu hayaridhishi hasa wapiganaji wa tabaka la chini jambo linalopunguza ari ya utekelezaji wa majukumu yao ya kuimarisha ulinzi na usalama katika Nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuangaliwa tena maslahi ya askari wa tabaka la chini ili nao waweze kutekeleza vyema majukumu yao kwa ufanisi zaidi na ari kubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini bado juhudi zinahitajika katika kuimarisha kilimo na ufugaji hasa kwa vile soko lipo katika kiwanda cha Bakhresa ila kiwango kinachohitajika cha Malighali za kiwanda hicho hakitoshelezi. Pia, kwa kuzingatia tunaitaka Zanzibar ya viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inavishauri Vikosi vyenye kujishughulisha na kilimo hasa JKU na Chuo cha Mafunzo kuhakikisha kwamba vinaimarisha kilimo ikiwa ni pamoja na kuyatumia vyema mashamba wanayoyamiliki ili kukuza uchumi nchini na kuepusha migogoro isiyo ya lazima kati ya vikosi hivyo na wananchi wanaoyatumia mashamba hayo; pia, kufanya kilimo na ufugaji uweze kuleta tija na maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba mradi wa ujenzi wa Gati haujatekelezwa kwa muda mrefu na una manufaa makubwa kwa Kikosi cha KMKM na nchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuzingatia suala la ujenzi wa Gati na Chelezo kwa ajili ya Kikosi cha KMKM ili waweze kufanikisha vyema utekelezaji wa majukumu yao ambayo kwa kiasi kikubwa hutegemea vitu hivyo kwa ajili ya shughuli zao na vyombo vyao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba kuna madeni mengi wanayoyadai Wakala wa Ulinzi JKU pamoja na Kampuni ya Ujenzi kwa huduma na kazi walizozitowa kwa taasisi mbali mbali zikiwemo taasisi za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kushughulikia kwa karibu na kuhakikisha kuwa taasisi zote zinazodaiwa na Wakala wa Ulinzi wa JKU pamoja na Kampuni ya Ujenzi kulipa madeni yao ili taasisi hizi ziweze kumudu kutekeleza vyema majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini majengo mengi ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi pamoja na vifaa vya kazi zao haviridhishi hata kidogo hasa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi katika Ofisi za Uwanja wa Ndege (Zanzibar Airport).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuhakikisha kuwa Vituo vyote vya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi vinafanyiwa matengenezo ili viweze kuwa na hadhi pamoja na kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi katika Vituo hivyo. Aidha, Kamati inasisitiza umuhimu wa kuimarisha huduma za Zimamoto na Uokozi katika

Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar, pia kuifanyia mapitio Sheria nambari *7* ya mwaka *1999* ya Kikosi cha Zimamoto.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa Sheria Nambari *1* ya mwaka *1980* ya Chuo cha Mafunzo ina mapungufu makubwa ambapo kwa sasa haiendani na mahitaji halisi ya utelekezaji wa kikosi hicho.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa chuo cha Mafunzo, Kamati inaishauri Serikali kuifanyia marekebisho Sheria nambari 1 ya mwaka *1980* ya kikosi hicho ili iendane na mahitaji halisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa vituo vya afya vya Vikosi vya SMZ kama KMKM Mtoni vinashindwa kutoa huduma kwa ufanisi wakati vinategemewa sana na wananchi wa maeneo mbali mbali ya Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuviimarisha vituo vya afya vilivyo chini ya Vikosi vya SMZ ikiwa ni pamoja na kutoa mgao wa dawa na vifaa tiba kutoka Serikali vyenye kutosheleza ili viweze kumudu utoaji huduma zinazostahiki kwa wananchi na hasa ikizingatiwa kwamba vituo hivyo vinahudumia wananchi kwa kiasi kikubwa mno.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba barabara ya kuelekea Makao Makuu ya Kikosi cha Valantia – Pemba hairidhishi hata kidogo na haipendezi kabisa kwa Kikosi kama hiki kuwa na barabara mbovu kama vile ilivyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuifanyia matengenezo barabara inayoelekea katika Makao Makuu ya Kikosi cha Valantia – Pemba ambayo ni mbovu mno na hasa katika kipindi cha mvua.

## PROGRAM KUU ZA URATIBU WA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (FUNGU D 07 – D 11)

**Mheshimiwa Spika,** katika programu kuu za Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa ujumla wake, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeona utekelezaji wa programu zinazosimamiwa na Tawala za Mikoa pamoja na Mamlaka ya Serikali za Mitaa zaidi katika ukusanyaji wa mapato pamoja na utatuzi wa kero mbali mbali za wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeona kuwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya ni mbovu na hazina hadhi kwa viongozi wetu kama hao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kutafuta utaratibu wa kujenga majengo kwa ajili ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya ambazo ama majengo yake ni mabovu au hayakidhi mahitaji ili kuwaondolea usumbufu viongozi na watendaji pamoja na wananchi wanaotumia majengo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini hakuna mfumo bora wa kudhibiti dawa za kulevya na uhalifu hasa ukizingatia kuwepo kwa kamati za ulinzi na usalama za Mikoa na Wilaya hadi shehia bado dawa za kulevya zinauzwa na kusambazwa kila siku na wauzaji na wasmbazaji hao wanafanya kazi hiyo bila ya wasiwasi na woga.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inazishauri Ofisi za Mikoa kuhakikisha kwamba zinadhibiti uingizaji wa dawa za kulevya katika mikoa yao hasa, kwa ile mikoa ya Pemba kwa vile inaonekana kuwa waingizaji wa dawa za kulevya wanakitumia Kisiwa cha Pemba kuingizia dawa hizo nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini katika eneo la Kuanikia na Kuuza Dagaa huko Fungu Refu, Mkokotoni hakuna huduma bora za afya, usalama wao ni mdogo na mazingira waliyonayo hayaridhishi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kupelekwa kwa huduma za msingi na zenye kutosheleza mahitaji kama vile kujengwa Kituo cha Polisi, Kituo cha Afya pamoja na vyoo katika eneo la Kuanikia na Kuuza Dagaa huko Fungu Refu, Mkokotoni, Unguja ambako kuna idadi kubwa ya waanikaji, wauzaji na wanunuzi wa dagaa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini uzembe mkubwa na uwajibikaji usioridhisha hata kidogo katika usimamizi mzima wa suala la migogoro ya ardhi na usimamizi bora wa matumizi ya ardhi hapa Zanzibar katika mikoa, wilaya na ngazi ya shehia hasa ukizingatia Serikali inalitilia mkazo sana usimamizi wa suala zima la utatuzi wa migogoro ya ardhi na usimamizi bora na matumizi ya ardhi ambapo hadi leo ujenzi holela umeshindwa kuzibitiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri na kuiomba Serikali kulitazama tena suala la usimamizi wa migogoro ya ardhi pamoja na usimamizi bora wa matumizi ya ardhi kwani kila uchao kutokana na kushindwa kuwa na mifumo bora ya matumizi ya ardhi na utatuzi wa migogoro ya ardhi, migogoro hiyo inaongezeka na uharibifu wa matumizi ya ardhi unaongezeka badala ya kupungua. Licha ya kuwa *Sheria ya Tawala za Mikoa, nambari 8 ya mwaka 2014* inawapa uwezo wa

kusimamia na kutatua migogoro ya ardhi, kitu ambacho wahusika kwa masikitiko makubwa wanashindwa kusimamia Sheria hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuna fedha zinazotolewa kwa ajili ya makundi maalum lakini fedha hizo hazileti manufaa kwa walengwa na pia hakuna mafunzo kabla ya kupewa fedha hizo wala mfumo bora wa utoaji wa fedha hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla, Serikali imejitahidi sana kutenga fedha kwa ajili ya kusaidia makundi maalum ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, hata hivyo, Kamati inashauri kutumiwa vizuri na kwa malengo yaliyokusudiwa fedha zilizotengwa ili makundi hayo yaweze kunufaika pamoja na kupatikana kwa matumizi halisi ya fedha hizo. Manufaa zaidi yawafikie walengwa wa fedha hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeona kwamba hakuna maeneo maalum kwa wafanyabiashara wadogo wadogo lakini hata yakitolewa Serikali inashindwa kuyasimamia na kuweka mifumo bora na mazingira yenye kuridhisha, mfano Kibandamaiti, Serikali yetu imejenga soko lakini sasa hivi hapafahamiki hakuna njia kila pahala pamejengwa vibanda bila ya utaratibu na mfumo maalum.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Wizara kuongeza juhudi za kuwatengea wafanyabiashara ndogo ndogo maeneo maalum kwa ajili ya kuendeshea shughuli zao ili kuondoa msongamano wa wafanyabishara ndogo ndogo na wananchi katika maeneo yasiyo rasmi kama vile eneo la Michenzani jumba nambari 7 na 8, hali inayowaondolea utulivu na faragha wananchi wanaoishi katika maeneo hayo pamoja na wapita njia.

## WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII (FUNGU D 12)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuna watu wasiokuwa wazanzibar na hawana vitambulisho, pia kuna ukiukwaji wa sheria katika utekelezaji wa jambo hili.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii umepanga kuimarisha Mfumo wa utoaji wa vitambulisho kwa ajili ya wafanyakazi wa taasisi za umma na binafsi na kuanza kutumia Mfumo wa Usajili wa Wakaazi wasiokuwa Wazanzibari baada ya kukamilika. Kamati inautaka Wakala kukamilisha Mfumo huo kwa muda uliowekwa ili huduma iliyokusudiwa iweze kupatikana.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia, nachukua fursa hii kuiomba jamii katika kipindi hiki cha mvua za masika zinazoendelea kunyesha kuzidi kuweka usafi wa mazingira yetu kwa kuitunza michirizi ya maji ya mvua na kuepuka kutupa taka kiholela ndani ya miji yetu, kufanya hivyo kutasaidia kujikinga na maradhi ya mripuko na malaria ambayo ni hatari kwa nchi yetu pamoja na kuitunza misingi hiyo ambayo inajengwa kwa kutumia fedha nyingi za Serikali na kuiweka miji yetu katika hali ya usafi.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, katika kukabiliana na mafuriko yanayotokea karibu kila mwaka katika maeneo mbali mbali ya Wilaya ya Magharibi *'A'* na *'B'*, Kamati inaishauri Serikali kujenga mitaro ya kupitishia maji katika maeneo hayo kama vile ilivyofanya katika maeneo ya Wilaya ya Mjini, Chake Chake, Wete na Mkoani.

**Mheshimiwa Spika,** pia, naomba niwashukuru Makamanda wa Idara Maalum za SMZ, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakurugenzi, Madiwani, Masheha na watendaji wote wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa utendaji, uzalendo wao na mashirikiano yao katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu katika kipindi chote cha maisha ya Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia Kamati imeona kwamba majukumu mengi ya taasisi za Serikali hayawezi kufanyika ipasavyo kutokana na kutoingiziwa fedha kwa wakati na kwa mujibu wa kilichopangwa katika bajeti zao. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati na kama zilivyopangwa ili ufanisi wa kiutendaji uweze kupatikana kwa maendeleo ya wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa, Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wairidhie, waichangie na waipitishe Bajeti hii na hatimae waidhinishe makadirio ya fedha zilizopangwa kutumiwa kwa mwaka wa fedha *2021/2022* kwa *Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati kwa kauli moja inaunga mkono uamuzi wa Serikali kuzirejesha taasisi zilizogatuliwa katika wizara zao za asili.

**Mheshimiwa Spika,** *Kwa Niaba ya Kamati yangu* **Naomba Kuunga Mkono Hoja.**

Ahsante,

**......................................**

**(Hassan Khamis Hafidh)**

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar**